

**Salamu za utangulizi zilizotolewa na Bw. Tumaini Mikindo, Mkurugenzi
Mtendaji wa PANITA kwa niaba ya Asasi za Kiraia katika mkutano watathmini
ya tatu ya utekelezaji wa mkataba wa lishe nchini ulioofanyika tarehe 24
Agosti, 2019 katika ukumbi wa Kambarage – Hazina jijini Dodoma**

1. Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mh. Selemani
Jafo – (Mb)
2. Mheshimiwa Katibu Mkuu - OR-TAMISEMI
3. Waheshimiwa Manaibu Makatibu Wakuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI
4. Washiriki kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais
5. Mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu
6. Wawakilishi wa Mawaziri
7. Waheshiwa Wakuu wa mikoa
8. Wawakilishi wa Wadau wa Maendeleo na Mashirika ya Umoja wa
Mataifa yaliyopo hapa Tanzania
9. Watendaji wa Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara
ya Afya
10. Wawakilishi kutoka vyombo mbali mbali vya Habari
11. Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana
12. Itifaki imezingatiwa

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa siku ya leo.

Aidha nitoe shukrani za dhati kwa niaba ya Asasi za kiraia kwa Mh. Waziri Kwa kutualika katika mkutano huu; na si hivyo tu na pia kutupa fursa ya kutoa salamu katika hadhara hii.

Hii ni uthibitisho tosha kwamba serikali ya awamu ya tano chini ya Mheshimiwa Raisi Dr. John Pombe Joseph Magufuli inavyothamini na kutambua mchango wa wadau ikiwemo Asasi za Kiraia katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa hili kuelekea uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo 2025. Mh. Waziri tunaomba utufikishie shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais.

Aidha nichukue fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan; kwa uongozi thabiti katika kuhakikisha swala la lische nchini linaimarika.

Vile vile nichukue fursa hii kukupongeza Mh. Waziri na watendaji wa wizara yako hususani kitengo cha lische kwa jitihada zenu katika kulisimamia suala hili muhimu kwa mustakabali wa taifa letu.

Mh. Mgeni rasmi, Kwa niaba ya Asasi za Kiraia nchini tunatoa pongezi kwa hatua zilizofikiwa katika uratibu wa masuala ya lishe kwa ngazi za mikoa na halmashauri. Hili linathibitishwa na matokeo ya tathmini mbili za awali zimeonesha maendeleo katika kupanga afua za lishe kwenye ngazi za Halmashauri na uratibu wa afua za lishe; mfano uwepo wa kamati za lishe kwenye kila Mkoa na Halmashauri, lakini pia kamati zinafanya vikao kwa zaidi ya 75% (Wastani wa vikao 3 kwa mwaka). Mh. Mgeni rasmi, kamati za lishe ni kiungo muhimu kwa wadau wote wa lishe, na zinafaida nyingi ikiwemo:

- i. Ndiyo namna bora ya uratibu wa masuala ya lishe kwa kuhusisha idara na makundi mbali mbali
- ii. Kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa watendaji wanaohusika
- iii. Kuongeza uwajibikaji wa kissekta na wadau wote wa lishe

Aidha baada ya kusema haya ningependa kuzungumzia mambo machache ambayo ni muhimu katika kuboresha utendaji kazi wa hizi kamati ili kuongeza tija katika harakati za kuboresaha uratibu wa wadau wa sekta ya lishe.

1. Utendaji kazi wa Kamati za lishe kwa ngazi za mikoa na halmashauri unakabiliwa na changamoto zifuatazo
 - i. Wajumbe mahususi wa kamati (Mwenyekiti na Wakuu wa Idara) kulingana na muongozo wamekuwa hawashiriki vikao

hivi kikamilifu; hali hii kwa asilimia kubwa inaathiri utendaji kazi wa kamati kwa sababu ya Wajumbe kubadilika badilika.

- ii. Baadhi ya idara ni ngeni kwenye masuala yanayohusu Lishe mfano; Idara ya uhasibu, hivyo zinahitaji ushirikiano wa karibu na Afisa lishe
- iii. Kukosekana kwa uelewa wa pamoja miongoni mwa wajumbe wa kamati hususani majukumu yao katika kamati ambako kunachangiwa na matumizi hafifu ya hadidu za rejea za kamati za lishe.

2. Mh. Mgeni rasmi tunaomba uweke msukumo wa makusudi kuhakikisha kuwa kamati zinaboresha utendaji kazi ili kulete tija; hii ikijumulisha Matumizi ya hadidu za rejea za kamati za lishe za Mikoa na Halmashauri Wajumbe waweke msukumo wa makusudi kwenye jambo hili hasa kutoka idara za mipango, Fedha na Uhasibu.

Aidha baada ya kusema maneno haya machache naishukuru serikali na Wizara yako kwa uamuzi wa kupeleka tathmini ya nusu mwaka ya makataba wa lishe katika ngazi ya mkoa, kwani itatoa fursa adhimu kwa wadau wakiongozwa na Waheshimiwa wakuu wa mikoa, tathmini ya kina juu ya mafanikio na

changamoto zinazowakabiri katika kuboreshaha hali ya lishe katika maeneo yao. Hii itasaidia kutoa suluhisho kwa ufanisi kubwa.

Mwisho, tunashukuru kwa kutushirikisha katika kikao hiki adhimu cha kujadili utekelezaji wa mkataba wa lishe.

Asanteni sana na asubuhi njema.